

TAARIFA YA IDARA YA

# Katibu wa Wachungaji na Huduma za Familia.

Pr. Switta E. Stevens

## UTANGULIZI

Kwanza kabisa nitoe shukrani zangu za dhati kwa Baba Mwumbaji wetu ambaye ametujalia kuufikia wakati mwingine kama huu. Niwashukuru sana viongozi wangu wa Konferensi kwa ukaribu na ushirikiano waliokuwa nao kwangu tangu nilipoitwa kusimamia idara hizi (September 22, 2022), pamoja na mabadiliko mengine yaliyojitokeza katikati ya safari yetu ya Kiutume, mfano, nilianza na idara ya Huduma Binafsi, katikati nikabadilishwa na kupewa huduma za kichungaji, na Huduma za Familia. Si hivyo tu, mgawanyo wa Konferensi ulipotokea, nimeongezewa majukumu mengine ya idara ya Uwakili na viambata vyake vyote; ninamtukuza sana Baba wa mbinguni kwa hayo yote. Ninawashukuru wakurugenzi wenzangu pamoja na watumishi wengine wote wa ofisi za makao makuu BWANA awabarikie sana. Ninatambua uhusika wa kundi maalum sana la wachungaji wa mitaa kwa namna tulivyofanya kazi kwa pamoja, na hata kuhakikisha kuwa taarifa hii inatokea ikiwa katika sura hii. BWANA Awabarikie sana.

Kwa kadri unavyoisikiliza taarifa hii, utagundua kuwa, ina mwangwi wa South Nyanza Conference ya kabla ya May 13, 2025 tulipokuwa pamoja na Mkoa wa Simiyu. Mabadiliko ya aina yo yote ile, yatakuwa machache kabisa yanayohusisha mwezi wa June 2025 baada ya SNC kubaki na Mkoa mmoja tu wa Mwanza bila kuhusisha wilaya za Sengerema, na Ukerewe.

Kwa upande mwingine taarifa hii itaangazia mambo makubwa manne: Uinjilisti, Uaminifu, Kubadili Taswira, na Uamsho na Matengenezo tuliyoanza nayo katika muhula huu mara tu baada ya Mkutano Mkuu wa 2022, na kuanza kutekelezwa rasmi kuanzia Januari 2023. Mambo haya makubwa, hata kama si yote, yataakisiwa katika dondoo zinazofuata katika muundo wa utekelezaji.

## HUDUMA ZA KICHUNGAJI


Hadi kufikia May 13, 2025, South Nyanza Conference ilikuwa na idadi ya wachungaji kazini 114 na wastaafu 9 katika mchanganuo ufutatao hapa chini:

| ***Eneo*** | ***Mitaani*** | | ***Chaplain Taasisi*** | | ***Ofisi Kuu*** | | ***Kwingine*** | | ***Jumla*** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Hadhi | Dumu | Mkataba | Dumu | Mkataba | Dumu | Mkataba | Dumu | Mkataba | |
| Mikono | 35 | 1 | 1 | 1 | 8 | | 2 | | 48 |
| Bila Mikono | 24 | 37 | 4 | 1 | | | | | 66 |
| ***Jumla*** | ***59*** | ***37*** | ***5*** | ***2*** | ***8*** | | ***2*** | | ***114*** |

Kwa kifupi kufikia May 13, 2025, SNC ilikuwa na Wachungaji wenye hati (Ministerial Credentials): 48, Wachungaji wenye Leseni (Ministerial License): 66, Wachungaji wastaafu wakiwa na hati zao za kichungaji: 9, Wachungaji

waliotengwa rasmi kwa kuwekewa mikono ni 8, Wachungaji waliostaafu: 1, Idadi ya Mitaa ni 97 na Wachungaji Wawili (2) walifariki dunia mwanzoni mwa mwaka 2024 na 2025.

## MAENDELEO YA MAFUNZO KIELIMU KWA WACHUNGAJI




*Jedwali 1: Jedwali hili huonesha idadi ya wachungaji na hadhi zao (elimu, uchungaji).*

## USTAWI WA WACHUNGAJI NA FAMILIA ZAO

Familia za Wachungaji zilizotembelewa: 110 kati ya 114

Familia za Wastaafu zilizotembelewa: 6 kati ya 10

Wachungaji 98% walihudhuria semina za Uamsho na Matengenezo almaarufu kama KUREJEA MADHABAHUNI May 17-25, 2024 kule Singida, matokeo yake kumekuwepo na uamsho Makanisani.

Kuundwa kwa Kamati maalum ya maombi yenye wajumbe 12, chini ya mwenyekiti Mch. Marko Barnabas ambayo imedumisha maombi kila siku saa 10:00 alfajiri tangu Juni 2024, hadi sasa.

Kama matokeo ya uamsho huo, roho 4968 ziliongolewa na kuletwa kwa Kristo kupitia huduma za kichungaji.

Tumefanikiwa kuongeza vituo vya Mikutano ya makambi kutoka vituo 166 2023 hadi kufikia vituo 196 kufikia Juni 2025.

Tumefaulu kupanga Makundi 103 kati ya 2022 hadi Juni 30, 2025.



*Picha 1: Mch. Switta E Stevens akipanga Kundi kuwa Kanisa mwezi Februari 2025.*

Kuanzia tarehe 27/03-06/04/2025, tumefaulu kuendesha semina na mafunzo maalum ya kichungaji yaliyowahusisha wachungaji/wachungaji mafunzoni, wazee wa Kanisa, pamoja na mashemasi katika vituo vya Bariadi, Mwanza, na Misungwi; ambapo wajumbe 696 walihudhuria katika mchanganuo ufuatao hapa chini:

| Idadi/Vituo | Wachungaji | Wazee Kanisa | Mashemasi | Wengine | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|
| BARIADI | 52 | 52 | 54 | 266 | 424 |
| MWANZA | 48 | 13 | 14 | 97 | 172 |
| MISUNGWI | 6 | 20 | 40 | 34 | 100 |
| ***Jumla Kuu*** | ***106*** | ***85*** | ***108*** | ***397*** | ***696*** |

*Jedwali 2: Jedwali hili huonesha mahudhurio ya mafunzo ya kichungaji: Bariadi, Mwanza, na Misungwi kuanzia March 27, 2025 hadi April 6, 2025, na May 1-3, 2025*

Tulikusudia kukutana na wachungaji wote wa mitaa 97, hata hivyo haikuwezekana kwani baadhi yao walikuwa masomoni hususani upande wa Simiyu. Idadi inayoonekana hapo ya wachungaji 106, inahusisha na wale wanaotumika katika ofisi za makao makuu.

Kwenye malengo yetu tulikusudia kuwafikia wachungaji wote. Hata hivyo kulingana na ratiba zilivyokaa, hatukufaulu kuwapata wote; tulifanikiwa kuwa na 92% ya wachungaji wote, yalikuwa ni mafanikio makubwa. Kwa upande wa wazee wa tulitazamia kuwa na uwakilishi wa Makanisa angalau

763 angalau mzee mmoja kutoka kila Kanisa, hata hivyo haikuwezekana, tulifaulu kuwa na wazee wa kanisa kama 11.1% hivyo haikuwa nzuri sana. Vivyo hivyo upande wa mashemasi, tulifaulu kuwa na 14% ya mashemasi tuliowatazamia. Idadi nyingine iliyobaki ilikuwa ya jamii ya waimbaji, na viongozi wengine.

Tumefanikiwa kutoa Makala kwa mchungaji kwa kila robo, hata kama hapo katikati mambo hayakuenda vizuri kulingana na mwingiliano wa majukumu. Makala hii imekusudiwa kuwatia moyo wachungaji, na kuleta chachu ya kuchunguza zaidi kuhusu utume wetu wa kichungaji.

## MPANGOKAZI IDARA YA HUDUMA ZA KICHUNGAJI (2026–2030)

| *Lengo Kuu* | *Lengo Mahususi* | *Matendo* | *Matokeo tarajiwa* | *Visashiria* |
|---|---|---|---|---|
| **Uamsho wa Kiroho** | Kuhimiza ukuaji wa kiriroho kwa wachungaji, wazee wa kanisa, mashemasi na viongozi wengine. | Mikutano ya kila mwaka ya kiroho; maombi ya kufunga ya robo, mwaka; usomaji wa Maandiko kwa mpango, nk. | Maisha ya maombi na uamsho thabiti miongoni mwa wachungaji, wazee wa kanisa na viongozi | 100% ya wachungaji wanashiriki katika mikutano ya kiroho; 70% ya makanisa,<br><br>Madhabahu za kifamilia kufikia 2030 |
| **Kuwezesha Viongozi** | Kuwajengea uwezo wachungaji, wazee, mashemasi, na viongozi wengine. | Semina maalum kwa wachungaji kila mwaka; mafunzo ya wazee na mashemasi, na viongozi wengine; kuhimiza mpango wa mafunzo endelevu ya wachungaji (CE). | Viongozi hodari, mahiri, wanaofanya kazi kitaaluma kama walivyojifunza | 80% ya wazee wamefundishwa kufikia kila mwaka, na 95% wachungaji wamekamilisha mafunzo yao ya kichungaji, na 15% wameongeza elimu zao kufikia 2030 |
| **Uinjilisti na Ukuaji wa Kanisa** | Kuimarisha uinjilisti kwa kuzingatia mbinu za Yesu (MH, 143) kufungua makundi na kupanda makanisa | Kampeni za uinjilisti kila mwaka; vikundi vidogo vidogo; mafunzo ya uinjilisti wa kidijitali; upandaji makanisa | Ongezeko la Makanisa mapya yanajiunga na udada wa makanisa, Konferensi na ulimwenguni. | 85% makanisa mapya kufikia 2030 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Malezi na matunzo ya waumini** | Kuimarisha, na kuboresha huduma za malezi na matunzo ya waumini wapya, na wale wa zamaini | Programu za malezi kwa kila mshiriki, kanisa, mtaa, na Konferensi; mafunzo ya Biblia kwa wanafunzi wa ubatizo; kampeni za kuwarejesha waliopotea | Waumini imara, thabiti wanaokua kiroho siku kwa siku, wasio na hofu ya nguvu za kishetani. | 95% ya waumini wanadumu kanisani, na 75% ya wanaopotea wanarejeshwa kufikia 2030 |
| **Ubora wa Familia za Wachungaji** | Kuimarisha na kuongeza ustawi wa familia za wachungaji | Makambi ya familia za kichungaji kila mwaka; semina za ndoa; kanda imara za kusaidiana kwa wake wa wachungaji | Familia za wachungaji bora, zenye afya, uthabiti, na uthubutu. | 100% ya familia za wachungaji zinahudhuria makambi ya familia za wachungaji kila mwaka kufikia 2030. |

## DIRA

Idara ya Familia kwa kipindi cha 2022 – 2025 imeongozwa na dira inayosema ***"Familia Imara, Jamii Imara."***

## MAFANIKIO MAKUU (2022–2025)

*Uinjilisti kupitia Huduma za Familia:*

Kupitia mkakati wa EEI kwa njia ya huduma za Familia uliozinduliwa rasmi na uongozi wa NTUC Januari 13, 2024, jijini Mwanza, na Januari 27, 2024 na uongozi wa SNC huko Bariadi, tulipangiwa kuwa na vituo 1030, na kubatiza roho 30,000 kuanzia March 17-April 13, 2024.




*Picha 1: Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Familia akitoa muelekeo wa Idara katika kushiriki mkakati wa EEI.*

Tulifanikiwa kuwa na vituo 734 na kubatiza roho 6196 changamoto kubwa ya kutofikia lengo hilo ilikuwa ni maandalizi hafifu hususani ya uinjilisti wa nyumba kwa nyumba unaoendana na mbinu ya Yesu Kristo.

Idara ya Huduma za Familia tulifanikiwa kufanya uinjilisti wa mahusiano na watu wa Imani tofauti hususani jamii ya Waislam mnamo February 24, 2024 ambapo Wakristo wa Waadventista wa Sabato na Waislam tulishirikiana kufanya usafi wa Soko kule Mwaloni Kirumba, na baadaye kuwa mkutano wa pamoja jioni katika uwanja wa CCM Kirumba.



*Picha 2: Baadhi ya viongozi wakishiriki katika program ya usafi pamoja na waislamu katika eneo la Kirumba.*

Kuanzia March 17-April 13, 2024, tulifanikiwa kuwa na kongamano maalumu la huduma za familia chini ya Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Familia (ECD) Dr. Winfrida Aneth Mitekaro zilizofanyika katika ukumbi wa The New Mwanza Hotel zikiwa na lengo la kukutanisha watu wa daraja la juu (The High-Profile People Group).

Kama matokeo, mtu mmoja alibatizwa akiunganishwa na kundi la watu saba kutoka kanisa la Kapripointi.




*Picha 3: Kutoka kushoto Dr. Winfrida Mitekaro, Pr. Davis Fue, Pr. Beatus Mlozi, Pr. Switta E Stevens, Pr. Onesmo Daniel na Eld. Mwita Machage katika Kongamano Maalum la Huduma za Familia lililofanyika Jijini Mwanza.*



*Picha 4: Mmoja wa wabatizwa katika hitimisho la Kongamano la Huduma za Familia lililofanyika Mwanza Hotel Jijini Mwanza.*

Makundi mbali mbali ya viongozi wa Dini yalialikwa wakiwemo kundi la Waislamu wasiopungua 130 walihudhuria.

Wachungaji wa madhehebu mbali mbali wakiwemo maasikofu na viongozi wa madhehebu na dini mbali mbali walivutiwa na Kongamano hilo. pia walialikwa kama njia ya kudumisha mahusiano yenye nia ya kutengeneza daraja la mawasiliano kuuendea utume wa kweli. Maaskofu 3, wa madhehebu ya Pentekostals, Anglican, na viongozi wengine walihusika.



*Picha 5: Baadhi ya Washiriki wa Kongamano Maalum la Huduma za Familia.*

Tumefanikiwa kuanzisha kituo cha mvuto chenye lengo la uinjilisti kwa kundi maalumu la watu wa daraja la juu (the high-profile people group. Kituo hiki kinaitwa Mwanza New Life Center ambacho kinakusudiwa kutumika kama Kanisa na mpaka sasa kinaendelea kikiwa na washiriki zaidi ya 50 waliojitolea kufanya uinjilisti kutumia mbinu za Yesu pekee. Matokeo yake tunayahifadhi lakini kuna watu maalum wanaendelea kuyatoa Maisha yao kwa Yesu.

Kituo hiki cha Mwanza New Life Center kimeungwa mkono na idara ya Huduma za Familia ya General Conference; kwa kutambua huduma zinazofanywa na kituo hiki, idara ilitoa mchango wake wa Milioni Kumi na Tatu (13M) kukisaidia kituo kuendesha utume kwa kutumia mbinu za Yesu Kristo (Tunasubiri utaratibu wa kukipanga kuwa Kanisa linalojitegemea hivi karibuni).

### *Malezi ya Mtoto wa Kiume (Parenting the Boy Child).*

Tumefaulu kuendesha semina maalum za malezi ya mtoto wa kiume katika vituo vikuu vitatu vya Bariadi, Mwanza, na Misungwi.

Mada zilizovuta usikivu wa wajumbe ni pamoja na, “Kwa nini mtoto wa Kiume, Kutambua makuzi ya mtoto wa kiume, Upekee wa mtoto wa kiume katika Biblia na katika jamii, Ulimwenguni lakini si wa ulimwengu, na Jukumu la Kanisa katika malezi ya mtoto wa kiume.”



*Picha 6: Washiriki wa Kanda ya Bariadi wakiwa katika moja ya Semina za Malezi ya Mtoto wa Kiume zilizofanyika Kanisa la Bariadi.*

Kitabu cha Mwongozo kwa ajili ya malezi ya mtoto wa kiume kimekuwa tayari, kitagawiwa makanisani hivi punde mara tu kitakapofika kwenye ofisi za Makao makuu.

MPANGO KAZI 2026 – 2030

| ***Lengo Kuu*** | ***Lengo Mahususi*** | ***Matendo*** | ***Matokeo yanayotarajiwa*** | ***Viashiria*** |
|---|---|---|---|---|
| Ndoa Imara zenye misingi ya Biblia | Kuimarisha ndoa katika familia za SNC | Kuwa na Makambi ya wana ndoa kila mwaka.<br><br>Semina za kila robo.<br><br>Kuimarisha ushauri wa kabla ya ndoa.<br><br>Masomo ya kifamilia | Ndoa imara, bora za wacha Mungu.<br><br>Wana ndoa wenye furaha na upendo.<br><br>Maandalizi bora ya wanaotarajia kuingia katika ndoa. | 100% ya wataradhia wa ndoa wamepata mafunzo kabla ndoa.<br><br>Makanisa 80% yanajihusisha na semina za ndoa kila robo kufikia 2030 |
| Uwezo wa Wazazi katika kulea Watoto | Kuwajengea wazazi uwezo wa kulea Watoto Kikristo, | Warsha za malezi ya watoto hususani mtoto wa kiume, na wa kike pia.<br><br>Vitabu vya malezi ya Watoto | Wazazi kama waalimu wa kwanza wa imani na dini wa watoto. | 80% ya Makanisa yanaendesha semina za Familia kila robo kufikia 2030 |
| Malezi ya vijana wadogo na vijana wakubwa | Kuwaandaa vijana kwa familia imara, na bora za Kikristo | Semina za usafi wa Maisha na uchumba wa Kikristo.<br><br>Programu za ulezi kwa vijana | Vijana wanaoishi sawa sawa na maadili ya Biblia | Kupinguza kama si kuondoa mimba kabla ya ndoa, na ndoa za utotoni kufikia 2030 |
| Uinjilisti kwa njia ya Familia za SNC | Familia kuwa vituo vya utume unaofuata mtindo wa Kristo | Kuwa na Wiki za uinjilisti wa kifamilia.<br><br>Huduma za kijamii. | Familia kuwa vituo vya uinjilisti; kila familia kuleta familia nyingine isiyo ya Kiadventista | Angalau 80% ya Makanisa yanaendesha program ya Uinjilisti wa Familia kufikia 2030 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Vikundi vya kifamilia | | |
| Familia zinazotoa huduma kwa Jamii. | Kuwa tayari kusaidia familia zinazokumbwa na au zilizo na changamoto | Ushauri wa talaka;<br><br>Usaidizi wa huzuni;<br><br>Elimu ya kupinga unyanyasaji wa kifamilia;<br><br>Vituo vya ushauri | Familia zilizovunjika kurejeshwa na kutiwa moyo kusonga mbele katika safari ya ndoa, na familia pia. | Kuwa na angalau kituo kimoja kila mtaa cha ushauri wa masuala ya Familia kufikia 2030 |

## SHUKRANI

Kwa mara nyingine naomba mniruhusu nimshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kutupatia nafasi ya kutumika, niwashukuru viongozi wangu, wachungaji wenzangu, pamoja na watenda kazi wengine wote kwa ushirikiano mkubwa walionipatia muda wote nikitumika ndani ya ofisi hizi. BWANA Awe pamoja nanyi nyote. Tumalizie na nukuu hii, "Wale wanaodumu katika kumwangalia Yesu, wakikua katika neema na kutafuta kuiga tabia Yake, watatiwa nguvu kusimama imara katika siku za mwisho" (5T., 213).

"TUKUTANE KWENYE UTUME."